# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU


*Simu: 255-262961500/1*
*Nukushi: 255-262961502*
*Baruapepe : press@ikulu.go.tz*
*Tovuti : www.ikulu.go.tz*

*OFISI YA RAIS,*
*IKULU,*
*1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,*
*CHAMWINO,*
*S.L.P 1102,*
*40400 DODOMA.*


***Dodoma***
***04 Februari, 2024***

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amesikitishwa na kifo cha Rais wa Jamhuri ya Namibia, Mhe. Dkt. Hage Gottfried Geingob.

Rais Samia amekuwa na urafiki wa muda mrefu na marehemu Mhe. Dkt Geingob, ambaye alikuwa anamuita kaka.

Rais Samia ametuma salaam za rambirambi kwa niaba ya Watanzania kwa wananchi wa Namibia, serikali ya nchi hiyo pamoja na mke wa marehemu, Bi Monica Geingos, na familia kwa ujumla.

"Nimesikitishwa sana na msiba wa kaka yangu Rais wa Namibia, Dkt. Geingob, ambaye nimemfahamu kuwa kiongozi msikivu, mtu wa watu na amekuwa miongoni mwa alama za ukombozi wa Namibia," Rais Samia amesema.

Kufuatia undugu na urafiki wa muda mrefu na Namibia, Rais Samia pia ametoa pole kwa uongozi na wanachama wote wa chama tawala rafiki cha SWAPO.

Mara ya mwisho Rais Samia alipokelewa kwa ukarimu mkubwa na Rais Geingob nchini Namibia tarehe 7 Mei, 2023 alipokwenda kuhudhuria mkutano wa dharura wa utatu wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC Troika).

Viongozi hao wawili walizungumzia mambo mbalimbali, ikiwemo kuimarisha ushirikiano baina ya nchi hizo mbili, hususan kisiasa na kiuchumi.

Tanzania na Namibia zimekuwa na uhusiano wa kindugu na wa muda mrefu tangu wakati wa harakati za ukombozi wa Taifa hilo. Aidha, uhusiano umeendelea kuimarika zaidi siku hadi siku.

Mungu ailaze roho ya Rais Dkt. Hage Gottfried Geingob mahali pema peponi, Amin

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu